



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA



TAREHE 18/02/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI ZA  
MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela anapenda kuwatangazia wananchi nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi katika Kata, Vijiji na Vitongoji vyote vilivyopo Wilaya ya Kyela.

**A. SIFA ZA WAOMBAJI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35
- ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea .
- iii. Awe anamiliki na uwezo wa kutumia simu janja (android) yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- iv. Awe na barua pepe (email address) na nywila (password) inayofanya kazi.
- v. Awe ana uwezo wa kusoma ramani za mitaa
- vi. Awe ni mkazi wa kata husika.

**B. KAZI NA MAJUKUMU**

- a. Kugawa au kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- b. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- c. Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi
- d. Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi

**C. MALIPO**

Malipo kwa siku ni shilingi 20,000/= kwa siku za kazi

**D. MAOMBI YA AMBATANISHWE NA:-**

1. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
3. Picha (passport size 2)
4. Barua ya maombi ipitie kwa Mtendaji wa Kata anayoishi

**E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**


Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu na barua pepe. Barua zote ziwasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa anwani ifuatayo.

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA,  
S. L. P 320.  
KYELA**

Aidha chini ya bahasha upande wa kulia iandikwe **AZM/KYL/2022/02**

**F. TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **24/02/2022 SAA 8:00 MCHANA**

  
Kenneth Nzilano  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**KYELA**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KYELA**